

JINA _____ NAMBARI _____ DARASA _____

KISWAHILI

KIDATO CHA TATU

MJARABU WA KWANZA

1. UFAHAMU

Wahenga walisema “motto umleavyo ndivyo akuavyo”. Hii in maana ya kuwa ukiogopa kutumia ufito kumchapa motto wako, ukamdekeza, utadeka na hatimaye ataharibika. Methali hii ina pacha yake ambayo ni “ukicha mwana kulia, utalia wewe.

Hizi ni methali zilizojaa busara kubwa. Mathalani, wewe ni mzazi au mtu yeyote mzima aliyetunukiwa madaraka juu ya watoto, lakini kila wanapokiuka uadilifu au mmoja wao anapokosea wewe unambembeleza tu, basi huwa unaizorotesha tabia yake. Mtoto huyo anaweza kuishia kuwa mtundu.

Hata hivyo, ni sharti tujue ya kwamba tuko katika nji apanda hapa. Kwa upande mmoja, zamani ilichukuliwa kwamba watoto n ahata mzima ana jambo la kuwaeleza, njia pekee ya kuliingiza katika ‘akili yao’ ni kuwatwanga ili kulikongomeza jambo hili. Ukweli ni kwamba akili ya motto si hafifu hata. Unaweza kusema ni kam ammea, ambao usiporutubishwa kimakusudi, ukapaliliwa vyem ana kustawishwa stahiki yake, basi hudhoofu; na mwisho kufifia .

Kwa upande mwingine, mtazamo wa kisas ani tofauti kabisa. Imethibitishwa ya kiwamba wanawake ni sawa kabisa katika maumbile yao wakilinganishwa na wanaume. Kwa jinsi hiyo, kweli wapo wanawake ambao hawana mwelekeo timamu kuhusu maisha, lakini ni kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu, basihawana akili. Kadhalika, si kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu basi hawana akili. Ama kwa kusema kweli binadamu yeyote huzaliwa na akilipungufu. Hili litokeapo, basi tunalikubali tu. Hatuwezi kumlaumu mtu kama huyo au muumba wake. Kwa hakika huu ndio msingi wa methali, “akili ni nywele, kila mtu an azake.” Vinginevyo, mtazamo wa kizamani ni taasubi kongwe tu za kiume zilizopitwa na wakati.

Aidha, kwa sababu watu wote huzaliwa na akili timamu, tene hawawi watu wazima kabla ya kuwa watoto kwanza, mtu mzima yeyote an ahali gani ya kuwadhulumu watotro na kujipambaniza na lawama za uongo dhidi ya vijana hao kwa madai kuwa hawana akili? Na je, ikiwa hawana akili, basi ndipo waonewe? Wanyanyaswe? Hii si jambo la busara. Kurudi Mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo. Kurudi kufaako ni kwa kupeleka, sio kwa kurudisha nyuma. Kurudi kuelekezako mbele ni kwa uongozi ambao lengo lake ni kumulikia mtoto kurunzi ilimradi kumwanguzia tariki njema.

Mtoto asinyimwe vya tunu vyovyote ambavyo ni stahiki yake, kwa kisingizio kuwa vimetengewa mtu mzima, ndugu mkubwa, mwalimu, au mtu awaye yeyote Yule aliyekabidhiwa jukumu la

kumlea au mtu mzima, ndugu mkubwa, mwalimu au mtu awaye yeyeto. Yule aliyekabidhiwa jukumu la kumlea au kumwogoza motto.

Mtoto ana haki ya kuhudumiwa kwa njia yeyote ifaayo ili akue na akili yake ikomae kikamilifu. Inafaa asomeshwe, apewe malezi bora ili naye alee wengine kistahiki.

MASWALI

- a) Mapenzi yasiyo kipimo yanaweza kuwa hatari kwa motto. Eleza kikamilifu huku ukirejelea habari uliyosoma. (Alama 3)

- b) Fafanua njia panda inayorejelewa na matunzi. (Alama 3)

- c) Mtoto analinganishwa na mmea katika taarifa hii, kwamba “usiporutubishwa kimakusundi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake basi hudhoofu,” tathmini kulinganishwa huku, huku ukirejelea taarifa. (Alama 3)

- d) Akili ni nywele, ‘Kila mtu ana ;zake. Eleza maana ya ndani ya methali hii kulingana na taarifa. (Alama 2)

- e) Onyesha kwamba unaelewa maana ya: (Alama 2)
Kurudi Mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo.”

f) Eleza maana ya: (Alama 2)

i) Kulikongomeza

ii) Kujipambaniza

2. MATUMIZI YA LUGHA. (Alama 30)

a. Eleza tofauti ya kimatamshi baina ya sauti zifuatazo.

i) (K)

ii) (G)

b. Eleza maana nne zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. (Alama 4)

Tande alimpigia milimo mpira

i)

ii)

iii)

iv)

c. Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu mwafaka. (Alama 3)

Hapa Kwetu Mna Siafu Wengi.

i)

ii)

iii)

iv)

d. Eleza maana ya ngeli. (Alama 1)

e. Andika sentensi mbili ili kuonyesha maana tofauti za alama ya kibainishi. (Alama 2)

- f. Eleza maana ya mofimu. (Alama 2)
- g. Eleza hali zinazodhihirika katika sentensi zifuatazo.
- i) Gari lake limebingirika mtaroni.

 - ii) Cha mlevi huliwa na mgema.
- h. Andika sentensi ifuatayo kwa usemi taarifa. (Alama 2)
“Hamjambo wanafunzi”, mwalimu aliwasalimia
- i. Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa. (Alama 2)
Watoto walinunuliwa viatu maridadi.
- j. Andika kinyume cha sentensi, (Alama 2)
Shangazi alifurahishwa na wimbo huo.
- k. Tunga sentensi kuonyesha maana ya vitale vifuatavyo. (Alama 2)
- i) Pamba

 - ii) Bamba
- l. Toa maelezo ya msamiati ufuatao. (Alama 4)
- i) Kielezi

ii) Kiiunganishi

iii) Kiwakilishi

3. ISIMU JAMII

a) Eleza maana ya. (Alama 5)

- i) Sajili.....
.....
- ii) Lahaja.....
.....
- iii) Isimu.....
.....
- iv) Lafudhi.....
.....

b) Eleza maana ya (Alama 5)
Kuchanganya ndimi

4. FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

a) Maigizo ni nini? (Alama 2)

b) Toa mifano mine ya maigizo. (Alama 4)

c) Taja Dhima nine za maigizo. (Alama 4)